Mzazi/Mlezi:

Kufika mwezi wa Novemba, kunamaanisha kujiandaa kwa ajili ya uwezekano wa hali mbaya ya hewa au dharura nyingine yoyote ambayo ineweza kusababisha wilaya ya shule kuwatuma watoto nyumbani mapema. Katika uwezekano huo wilaya itawajulisaha wazazi kwa njia ya simu. Kwa hivyo ni muhimu sana shule ya mtoto wako kuwa na taarifa za karibuni za jinsi ya kuwasiliana nawe.

Kama namba ya simu ya nyumbani, simu ya mkononi, simu ya kazi au simu ya dharura yako zimebadilika, tafadhali chukua muda kuwasiliana na shule ya mtoto wako (314).

Pia, tunawauliza wazazi wahakikishe kwamba habari za karibuni kuhusu watu wazima wanaoruhusiwa kumchukua mtoto wako katika hatari, ziko kwa faili ya shule. Mzazi wa mtoto au mtu mzima aliyetambulishwa na mzazi, tu, wanaruhusiwa kumchukuwa mototo wako.

Wazazi wanakumbushwa kuwa na mpango palipo na uwezekano wa watoto kuachiliwa mapema, hali ya hewa au dharura nyengine. Mpango huu uzingatie mahali pa kuwaacha watoto wako wadogo.

Wilaya pia inauliza wazazi kujiepusha na wito wa shule panapokuwa na hali mbaya ya hewa, inayosababisha watoto kuachiliwa mapema. Simu za shule zote zitatumiwa kwa ajili ya mawasiliana ya dharura.

Wilaya inapoamua kufanga shule au kuwaachilia watoto mapema, kutokana na hali mbaya ya hewa au dharura nyengine, taarifa hiyo itapatikana kwa tovuti ya wilaya katika www.slps.org, ukurasa wa Facebook ya wilaya na akaunti ya Twitter katika @SLPS_INFO. Taarifa hii itapewa stesheni za televisheni za mji huu: KTVI, KMOV, KSDK, KPLR na KMOX.

Tunakushukuru kwa kutusaidia na njia za kuwasiliana nawe.

Dhati,

Principal
School Name
Phone Number